

*Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Manispaa ya
Tabora)*

Tangazo la Serikali Na. 360

TANGAZO LA SERIKALI NA. 360 la tarehe 4/9/2015

**SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA (2002)
(SURA 290)**

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu Na.6 (1) na 16 (1)

SHERIA NDOGO YA (USHURU WA HUDUMA YA YA HALMASHAURI YA MANISPAA
YA TABORA, 2014

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za ushuru wa Huduma ya Mji za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, 2014 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Tafsiri

3. Katiba Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itatamkwa vinginevyo:

“Halmashauri” maana yake Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

“Kampuni Mkazi la Biashara” maana yake ni kila Kampuni lililosajiriwa au ambalo halijasajiriwa na au Wakala wa Kampuni ambalo linafanyakazi ndani ya eneo la Utawala la Mamlaka.

“Kampuni lililosajiliwa” maana yake ni mtu yejote awe Kampuni, muunganiko wa Biashara na au ubia ulioruhusiwa kisheria kufanya kazi kama mtu mmoja.

*Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Manispaa ya
Tabora*

Tangazo la Serikali Na. 360

“Kampuni: lisilosajiliwa” maana yake ni Kampuni lolote ambalo ni tofauti na Kampuni lililosajiriwa na itajumuisha mtu anaefanya biashara kwa jina la Biashara (Sole proprietor) na Mtu binafsi.

“Manispaa” maana yake ni sehemu yeoyote ya ardhi iliyondani ya mipaka ya Manispaa.

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya aliyeajiriwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

**Ushuru/
Kodi** 4. Kutakuwa na ushuru wa Huduma utakaolipwa na kukusanywa kutoka katika Kampuni lililosajiriwa na Kampuni lisilosajiriwa kwa kila mwaka wa mapato ambao ni asilimia tatu 0.3% kwa pato la mwaka katika shughuli zote zinazojumuisha utengenezaji, uzalishaji (Manufacturing, Processing), uzalishaji wa kilimo, ugawaji wa bidhaa, kutoa huduma, biashara, uingizwaji wa bidhaa au huduma ndani ya eneo la utawala la mamlaka.

**Ukiukaji
wa Sheria
Ndogo** 5. Ikiwa Kampuni mkazi la biashara, kampuni lililosajiliwa na kampuni lisilosajiliwa litakiuka Sheria Ndogo hii litatozwa adhabu isiyozidi asilimia ishirini na tano (25%) ya pesa ambayo alitabiwa kulipa.

Makosa 6. Kila kampuni mkazi la biashara, Kampuni lililosajiriwa na Kampuni lisilosajiriwa litakalokataa/litakaloshindwa kulipa ushuru au kodi kutokana na Sheria Ndogo hii litakuwa limetenda kosa na litatakiwa kulipa adhabu isiyozidi asilimia ishirini na tano ya pesa ambayo alitakiwa kulipa na ushuru/pasa ambayo alitakiwa kulipa.

Adhabu 7. Mtu au Kampuni yoyote itakayokwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi itakuwa imetenda kosa na ikipatikana na hatia itatozwa faini isiyozidi shillingi elfu hamsini(50,000) au kifungo cha miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

*Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Manispaa ya
Tabora*

Tangazo la Serikali Na. 360